

Hitimisho:

Kwenye ukanda wenye mvua mvua kiasi, nyasi aina ya *B. decumbens* cv Basilisk zinaonekana kufanya vizuri katika tabia za ukuaji na wingi wa mavuno. Wakulima wa nyasi wafuate hali ya hewa katika kuchagua nyasi stahiki.



Tabia za ukuaji wa nyasi aina ya *Brachiaria* katika ukanda wa juu wa nyada za kusini mwa Tanzania (Rungwe).

*Ismail S. Selemani, Dismas Mwaseba, Amur Nyambilila, Joseph Hella, Athumani Kyaruzi, Susan Nchimbi, Camilus Sanga.

Utangulizi

Ufugaji nchini Tanzania unakabiliwa na uhaba wa malisho na hivyo kusababisha kushuka kwa uzalishaji wa maziwa. Tafiti zilizotangulia zinaonesha kuwa uzalishaji kwa sasa ni kati ya lita 4 hadi 8 badala ya lita 15 kwa ng'ombe kwa siku (Mtengeti na wengine 2018).



Mradi wa InnovAfrica ulianzisha majaribio ya uzalishaji wa nyasi aina ya *Brachiaria* katika wilaya ya Rungwe (shamba la kijiji Ilenge na shamba la Msigwa) na Morogoro (shamba la Magadu) kwa lengo la kutafiti tabia za ukuaji na wingi wa mavuno. Aina tatu za *Brachiaria* zilihusishwa katika majaribio yaliyofanyika kwa miaka mitatu mfululizo kuazia 2017 hadi 2020.

Horizon 2020
European Union funding
for Research & Innovation



Njia za utafiti

Upandaji na ukusanyaji wa takwimu ulifuata taratibu zote za kisanyansi; i) kupanda kwa mistari, ii) kupanda kwa wakati iii) Kuhesabu mimea iliyoota, iv) Kuhesabu vichipukizi v) kupima urefu wa mimea na vii) kupima wingi wa mavuno.



Matokeo ya utafiti:

Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa maeneo yenye mvua ya wastani (sub-humid condition) yanafanya vizuri katika ukuaji wa nyasi aina ya *Brachiaria* ukilinganisha na maeneo ya nyanda za juu kusini (humid). Kadhalika *Brachiaria decumbens* cv Basilisk imefanya vizuri ikilinganishwa na aina zingine.



Jedwali la 1: Tabia za ukuaji wa nyasi aina ya *Brachiaria Rungwe* na Morogoro

	<u>Idadi ya mimea</u>	<u>Idadi ya vichipukizi</u>	<u>Urefu wa mmea</u>
<u>Ilinge VKC (Mvua nyingi)</u>	71.84 ± 2.99a	3.85 ± 0.35c	77.94 ± 2.75b
<u>Msigwa Farm (Mvua nyingi)</u>	77.54 ± 3.07a	5.19 ± 0.36b	84.51 ± 2.84b
<u>Magadu Farm (Mvua wastani)</u>	70.27 ± 2.98b	7.94 ± 0.35a	120.12 ± 2.74a
<u>Utafauti wa kitakwimu (5%)</u>	*	***	**
<u><i>B. decumbens</i> CV. Basilisk</u>	127.75 ± 3.44a	6.19 ± 0.40a	70.31 ± 3.17ab
<u><i>B. brizantha</i> CV. Xaraes</u>	80.08 ± 3.44b	4.68 ± 0.40b	78.41 ± 3.31a
<u><i>B. brizantha</i> CV. Piata</u>	81.65 ± 3.46b	4.86 ± 0.40b	86.25 ± 3.84b
<u>Utafauti wa kitakwimu (5%)</u>	**	**	*

Wingi wa mavuno: *B. decumbens* cv Balisisk inaonekana kufanya vizuri kwenye wingi wa mavuno katika nyanda zote.

